Vitu Vilivyoonekana Ndani Ya Paulo

na

Ellis P. Forsman

Vitu Vilivyoonekana Ndani Ya Paulo

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Vitu Vilivyoonekana Ndani Ya Paulo

Fil. 4:9

Maelezo ya Baba yetu wa mbinguni maranyingi ilivyotumiwa na Paulo ni "*Mungu wa amani*".

- Rum. 15:33, "*Mungu wa amani awe pamoja nanyi nyote. Amen.*"
- Rum. 16:20, "*Naye Mungu wa amani atamseta shetani chini ya miguu yenu upesi, Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja nanyi [Amina]*"
- 2 Kor. 13:11, "*Hatimaye ndugu kwaherini, mtimilike, mfarijike, nieni mamoja, make katika amani; na Mungu wa upendo na amani atakuwa pamoja nanyi.*"
- 1 Thess. 5:23, "*Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo.*"
- Ebr. 13:20, "*Basi Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka katika wafu Mchungaji Mkuu wa kondoo, kwa damu ya agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu.*"

Katika mtindo unaofanana Paulo anamuelezea Mungu katika Fil. 4:9 ambayo tunatumia kama kifungu cha somo letu.

Fil. 4:9, "*Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi.*"

Katika kifungu chetu, tunajifunza kwa Paulo ufunguo wa kuwa na "*Mungu wa amani*" akitubariki katika maisha yetu.

Inajumuisha kufanya "vitu"…

- Kujifunza kutoka kwa Paulo.
- Kupokea kutoka kwa Paulo.
- Kusikia kuhusu Paulo.
- Kuonekana ndani ya Paulo.

Ni baadhi ya vitu gain "vilivyoonekana ndani ya Paulo", ambazo tukifanya, itatuakikishia kwamba "*Mungu wa amani*" atakuwa pamoja nasi?

Jibu linaweza kupatikana katika nyaraka zake zote kwa Wafilipi na katika barua zake zingine. Kwa mfano, tunaona…

Kuhusika kwake kwa ajili ya ndugu zake

Kama ilivyoelezewa katika Wafilipi.

Kwa swala la Euodia na Sintike.

Fil. 4:1-3, "*Basi ndugu zangu wapendwa wangu ninaowaonea shauku, furaha yangu na taji yangu, hivyo simameni imara katika Bwana, wapenzi wangu. Namsihi Euodia, namsihi na Sintike wawe na nia moja katika Bwana. Naam, nataka na wewe pia mjoli wa kweli, uwasaidie wanawake hao; kwa maana waliishindania Injili pamoja nami, na Klementi naye, na wale wengine waliotenda kazi pamoja nami, ambao majina yao yamo katika kitabu cha uzima.*"

Hakika, pamoja na ndugu wote pale Filipi.

Fil. 1:8-11, "*Maana Mungu ni shahidi wangu jinsi ninavyowaonea shauku ninyi nyote katika moyo wake Yesu Kristo. Na hii ndiyo dua yangu kwamba pendo lenu lizidi kuwa jingi sana, katika hekima na ufahamu wote; mpate kuyakubali yaliyo mema; ili mpate kuwa na mioyo safi, bila kosa, mpaka siku ya Kristo; hali mmejazwa matunda ya haki, kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu.*"

Kwingineko, Paulo anafunua kujali kwake.

Kwa makanisa yote.

2 Kor. 11:28-29, "*Baghairi ya mambo ya nje, yako yanijiayo kila siku, ndiyo maangalizi ya makanisa yote. Ni nani aliye dhaifu nisiwe dhaifu nami? Ni nani aliyekwazwa nami nisichukiwe?*"

Kwa ndugu ambao ni dhaifu katika imani.

- 1 Kor. 8:8-13, "*Lakini chakula hakituhudhurishi mbele za Mungu; maana tusipokula hatupunguziwi kitu, wala tukila hatuongezewi kitu. Lakini angalieni huu uwezo wenu usije ukawakwaza wale walio dhaifu. Kwa maana mtu akikuona wewe uliye na ujuzi, umeketi chakulani ndani ya hekalu la sanamu, je! Dhamiri yake mtu huyo, kwa kuwa yu dhaifu, haitadhibitika hata yeye naye ale vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu? Na yule aliye dhaifu aangamizwa kwa ujuzi wako, naye ni ndugu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake. Hivyo mkiwatenda dhambi ndugu zenu na kuitia jeraha dhamiri iliyo dhaifu, mnamtenda dhambi Kristo. Kwa hiyo,*

chakula kikimkwaza ndugu yangu, hakika sitakula nyama hata milele, nisije nikamkwaza ndugu yangu."

- Rum. 14:14-21, "*Najua tena nimehakikishwa sana katika Bwana Yesu, ya kuwa hakuna kitu kilicho najisi kwa asili yake, lakini kwake yeye akionaye kitu kuwa najisi, kwake huyo kitu kile ni najisi. Na ndugu yako akiingia huzuni kwa sababu ya chakula , umeacha kwenda katika upendo. Kwa chakula chako usimharibu mtu yule ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake. Basi huo wema wenu usitajwe kwa ubaya. Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu. Kwa kuwa yeye amtumikiaye Kristo katika mambo hayo humpendeza Mungu, tena hukubaliwa na wanadamu. Basi kama ni hivyo, na mfuate mambo ya amani na mambo yafaayo kwa kujenga. Kwa ajili ya chakula usiiharibu kazi ya Mungu. Kweli vyote ni safi; bali ni vibaya kwa mtu alaye na kujikwaza. Ni vyema kutokula nyama wala divai wala kutenda neno lo lote ambalo kwa hilo ndugu yako hukwazwa.*"

- Rum. 15:1-3, "*Basi imetupasa sisi tulio na nguvu kuuchukua udhaifu wao wasio na nguvu, wala haitupasi kujipendeza wenyewe. Kila mtu miongoni mwetu na ampendeze jirani yake, apate wema akajengwe. Kwa maana Kristo naye hakujipendeza mwenyewe; bali kama ilivyoandikwa, Malaumu yao waliokulaumu wewe yanipata mimi.*"

Kujitahidi kwake kwa ajili ya ukamilifu

Kwa Wafilipi, Paulo aliandika:

Kwa kukubali kwake kwamba hakuwa mkamilifu.

Fil. 3:12, "*Si kwamba nimekwisha kufika, au kwamba nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu.*"

Hamu yake ya kuendelea mbele, kufika mbele, kufikia malengo.

Fil. 3:12-14, "*Si kwamba nimekwisha kufika au kwamba nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu. Ndugu sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo niifikie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.*"

Kwa kanisa la Korintho, Paulo anasema…

Kwamba aliona maisha yake ya Ukristo kama "mbio", "mchezo wa ngumi".

1 Kor. 9:24-26, "*Je! Hamjui ya kwamba wale washindanao kwa kupiga mbio, hupiga mbio wote lakini apokeaye tuzo ni mmoja? Pigeni mbio namna hiyo ili mpate. Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika. Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo si kama asitaye; napigana ngumi vivyo hivyo, si kama apigaye hewa;*"

Mahali ambapo mara zote kuna nafasi ya maendeleo, asije akawa "hajaitimu".

1 Kor. 9:27, "*Bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; iswe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.*"

Kwa nini awe na hamu ya ukamilifu? Kama ilivyoelezwa katika Fil. 3:8-11, ilikuwa sehemu ya "mtazamo wake mhimu" kumpata Kristo na kukutwa ndani Yake."

Tukitaka vivyo hivyo kwetu sisi, hivyo tunapaswa kuwa na nia kama hiyo.

Kitu kingine ambacho kilionekana ndani ya Paulo ambayo inafanana kwa ukaribu na nia hii ya ukamilifu ni…

Juhudi zake za kuwaokoa waliopotea.

Kama alivyoeleza katika Waraka Wake Kwa Wafilipi.

Juhudi zake za kuendelea bila kujali kuwepo kifungoni ndani ya nyumba.

Fil. 1:12-14, "*Lakini ndugu zangu nakata mjue ya kuwa mambo yote yaliyonipata yametokea zaidi kwa kuieneza Injili; hata vifungo vyangu vimekuwa dhahiri katika Kristo, miongoni mwa askari na kwa wengine wote pia. Na wengine wa hao ndugu walio katika Bwana, hali wakapata kuthibitika kwa ajili ya kufungwa kwangu, wamezidi sana kunena neno la Mungu pasipo hofu.*"

Kwa mapenzi yake angejitoa mwenyewe kama dhabihu kama ingesaidia.

Fil. 2:17, "*Naam, hata nikimiminwa juu ya dhabihu na ibada ya iamni yenu, nafurahi; tena nafurahi pamoja nanyi nyote.*"

Kiwango ambacho angefikia inaonekana katika waraka wake kwa Wakorintho.

Alifanyika mtumishi wa wote.

1 Kor. 9:19-23, "*Maana ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi. Nalikuwa kama Myahudi wa Wayahudi, ili nipate Wayahudi; kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa kama chini ya sheria, (ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria), ili niwapate walio chini ya sheria. Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria, (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo), ili niwapate hao wasio na sheria. Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu. Nami nafanya mambo yote kwa ajili ya injili ili kuishiriki pamoja na wengine.*"

Alipitia mateso mengi kama mtumishi wa Kristo na Injili Yake.

2 Kor. 11:23-27, "*Wao ni wahudumu wa Kristo? (Nanena kiwazimu), mimi ni zaidi katika taabu kuzidi sana; katika mapigo kupita. Kwa Wayahudi nalipata mapigo arobaini kasoro moja. Mara tatu nalipigwa kwa bakora; mara moja nalipigwa kwa mawe; mara tatu nalivunjikiwa jahazi; kuchwa kucha nimepata kukaa kilindini; katika kusafiri mara nyingi hatari za mito; hatari za wanyang'anyi; hatari kwa taifa langu; hatari kwa mataifa mengine; hatari za mji; hatari za jangwani; hatari za baharini; hatari kwa ndugu za uongo; katika taabu na masumbufu; katika kukesha mara nyingi; katika njaa na kiu; katika kufunga mara nyingi; katika baridi na kuwa uchi.*"

Hata pamoja na mates ohayo katika juhudi zake za kuwaokoa wengine, bado tunaona kitu kingine ndani ya Paulo ambayo ni nzuri kuiga…

Furaha yake katika mateso

“Furaha” hii kimsingi inaonekana katika waraka kwa Wafilipi.

Ambayo tumeona mara nyingi na pia ni “waraka wa furaha”.

Kwa mfano, furaha yake katika Kristo inahubiriwa, bila kujali kufungwa kwake na juhudi za wahubiri wa uongo.

Fil. 1:12-18, “*Lakini ndugu zangu nataka mjue ya kuwa mambo yote yaliyonipata, yametokea zaidi kwa kuieneza injili; hata vifungo vyangu vimekuwa dhahiri katika Kristo, miongoni mwa askari na kwa wengine wote pia. Na wengi wa hao ndugu walio katika Bwana, hali wakapata kuthibitika kwa ajili ya kufungwa kwangu, wamezidi sana kunena neno la Mungu pasipo hofu. Wengine wanahubiri habari za Kristo kwa sababu ya husuda na fitina; na wengine kwa nia njema. Hawa wanamhubiri kwa pendo, wakijua ya kuwa nimewekwa ili niitetee Injili; bali wengine wanamhubiri Kristo kwa fitina, wala si kwa moyo mweupe, wakidhani kuongeza dhiki za kufungwa kwangu. Yadhuru nini? Lakini kwa njia zote ikiwa ni kwa hila, au ikiwa ni kwa kweli, Kristo anahubiriwa; na kwa hiyo nafurahi, naam, nami nitafurahi.*”

Hata kama ingemaanisha kifo, aliitazama kama sababu ya kufurahi, na aliwataka wafurahi pamoja naye.

Fil. 2:17-18, “*Naam, hata nikimiminwa juu ya dhabihu na ibada ya imani yenu, nafurahi; tena nafurahi pamoja nanyi nyote. Nanyi vivyo hivyo furahini, tena furahini pamoja nami.*”

Katika Warumi, alieleza sababu ya “kufurahi katika shida”.

Majaribu kama hayo na mateso yangesababisha “**uvumilivu”.**

Rum. 5:3, “*Wala si hivyo tu, ila nafurahi katika dhiki pia, mkijua ya kuwa dhiki kazi yake ni kuleta saburi;*”

Ambayo badala yake ingesababisha “tabia” na “Tumaini”

Rum. 5:4, “*Na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo, na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini.*”

Mwisho

Haya ndiyo mambo bora yaliyoonekana ndani ya Paulo, ambayo nasi tunajifunza kutoka kwake kama tukichukulia maanani nyaraka zake.

Pia tunapaswa, kama tuna mtamani "*Mungu wa amani*" kuwa pamoja nasi na kwa hakika alikuwa pamoja na Paulo maisha yake yote na utumishi kama nidhamu kwa Yesu Kristo!

Je vitu vilivyoonekana kwa Paulo, vinaonekana kwetu? Je tunaishi katika njia ambayo tunaweza kuwaambia wengine:

Fil. 4:9, "*Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi.*"

Kwa mtazamo wa vifungu kama 1 Tim. 4:12 na Tito 2:6-7, ambapo tunaitwa kuwa kama mfano wa wengine, tunapaswa!

- 1 Tim. 4:12, "*Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi.*"
- Tito 2:6-7, "*Vivyo hivyo na vijana waume uwaonye kuwa na kiasi; katika mambo yote ukijionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema, na katika mafundisho yako ukionyesha usahihi na ustahivu,*"

Na "Mungu wa amani" atusaidie kuishi kwa njia ambayo tunaweza kuwa mfano kama Paulo!